

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI



TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji anatangaza **nafasi 500** za ajira kwa vijana wa Kitanzania waliohitimu Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (**JKT**) au Jeshi la Kujenga Uchumi (**JKU**) walioko makambini au nje ya makambi. Aidha, waombaji wote wanapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

1. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe raia wa Tanzania;
- ii. Awe amehudhuria na kuhitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) waliopo Makambini au tayari amerudi Uraiani;
- iii. Awe hana ajira au hajawahi kuajiriwa na Taasisi yoyote Serikalini;
- iv. Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya awali ya Jeshi la Uhamiaji;
- v. Awe na Cheti cha Kuzaliwa;
- vi. Awe na Kitambulisho cha Taifa au Nambari ya Utambulisho iliyotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) au Kitambulisho cha Mzanzibari;
- vii. Awe na siha njema ya mwili na akili iliyothibishwa na Daktari wa Serikali,
- viii. Awe hajawahi kutumia Dawa za kulevya.
- ix. Asiwe na Kumbukumbu au Taarifa zozote kuhusika katika matukio au masuala ya Kiharifu;
- x. ;Asiwe na alama yoyote au michoro (Tattoo) katika mwili wake;
- xi. Awe hajaoa au kuolewa wala kuwa na mtoto;
- xii. Awe tayari kufanya kazi mahali popote nchini Tanzania;
- xiii. Mwombaji mwenye Elimu ya Kiwango cha Shahada au Stashahada ya Juu au Stashahada au Astashahada anatakiwa kuwa na umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 30; katika moja ya fani zifuatazo:- Uhandisi Mkadiriaji Majenzi (QS), Msanifu Majengo (Architect), Wataalam wa Lugha (Kifaransa, Kihabeshi, Kiarabu, Kihispaniola, Kitaliano, Kichina na Mawasiliano ya watu wenye mahitaji maalum – **Lugha za Alama**), Msanifu Mifumo ya Kielektroniki {System Developers}, Usalama wa Mifumo (Cyber or System Security), *Software Developers and Programmers*, na *Busines System Analysts* au Wanamaji (Maritime Technology), *Electronics and Telecommunications*, *Mechanics*; pamoja na fani kama Saikolojia, Sheria, Ugavi na Ununuzi, Uhasibu au Usimamizi wa Fedha, Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, na Takwimu.

- xiv. Mwombaji wa Kidato cha Sita au cha Nne awe mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 28. Aidha, mwombaji anapaswa kuwa na Cheti cha Taaluma kutoka katika Vyuo mbalimbali vinavyotambuliwa na Serikali katika fani zifuatazo:- Umeme, Ushonaji, Ufundi wa Magari, Ufundi Mitambo, Ufundi wa Viyoyozi (AC), Udereva, Ukatibu Muhtasi (Secretarial), Utunzaji wa Kumbukumbu, Ufundi Seremala, Ufundi Bomba, Uhandisi wa Sauti (Sound Engineering), Uchapaji (Printing Technician) na Usanifu Michoro (Graphic designing). **Ikumbukwe kuwa Waombaji wenye Fani tajwa hapo juu watapewa kipaumbele.**
- xv. Awe tayari kufanya kazi za Idara ya Uhamiaji mahali popote Tanzania.
- xvi. Awe tayari kujigharimia katika Hatua zote za ufuatiliaji na uendeshwaji wa zoezi hili la Ajira.

2. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:

Mwombaji anatakiwa kuandika barua ya Maombi ya ajira kwa mkono wake pamoja na namba ya simu anayoweza kupatikana muda wote. Pamoja na barua ya maombi, anapaswa pia kuambatisha nyaraka zifuatazo:-

- i. Barua ya Utambulisho toka Mtendaji Kata au Serikali ya Mtaa/Kijiji au Shehia;
- ii. Waombaji waliopo Makambini, barua zao zipitie kwa Wakuu wa Kambi husika;
- iii. Nakala ya Cheti cha kuhitimu Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU);
- iv. Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa;
- v. Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au nambari ya Utambulisho kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa au Kitambulisho cha Mzanzibari;
- vi. Nakala ya vyeti vya kuhitimu shule (Leaving Certificates) na vyeti vya Taaluma (Academic Certificates);
- vii. Nakala ya vyeti vingine vya Fani mbalimbali;
- viii. Wasifu wa Mwombaji (CV);
- ix. Picha Nne (04) (Passport size) zenye rangi ya bluu bahari;

MUHIMU NA LA KUZINGATIA: Nakala za Vyeti vyote vithibitishwe na Kamishna wa Viapo au Hakimu.

3. MAOMBI YA AJIRA YATUMWE KWA ANUANI ZIFUATAZO:

- a) Waombaji waliopo Tanzania Bara watume maombi yao kwa:-

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji,
4 Barabara ya Mwangosi,
Uzunguni,
S. L. P. 1181,
DODOMA.

b) Waombaji walioko Zanzibar watume maombi yao kwa:-

Kamishna wa Uhamiaji,
Afisi Kuu,
S. L. P. 1354,
ZANZIBAR.

4. Mwisho wa kupokea maombi ya ajira ni tarehe 29 Disemba, 2022.

5. TAHADHARI;

- i. ***Ikumbukwe kuwa, barua zitakazowasilishwa kwa mkono hazitapokelewa.***
- ii. ***Mwombaji yoyote atakayebainika kuwasilisha nyaraka za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa Mahakamani.***

Imetolewa na,

**KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI,
MAKAO MAKUU YA IDARA YA UHAMIAJI,
S. L. P. 1181
DODOMA
TAREHE: 11/12/2022**